**Historia ya wanafunzi waliopata ujauzito kurudi shule.**

Baada ya kupata uhuru, Rais Julius K. Nyerere aliamini ili kuondokana na changamoto zinazokabili na kuchochea maendeleo elimu ndio chombo kikuu kinachoweza kutumika kukabiliana na changamoto hizo, zikiwemo umaskini, maradhi na ujinga. https://www.juliusnyerere.org/uploads/uamuzi_wa_busara.pdf

Tulianzisha Sheria ya Elimu ya Taifa ya mwaka 1978 kupitia msukumo wa Nyerere wa elimu nchi nzima. Sheria hii haikujumuisha kifungu chochote chenye ubaguzi katika haki za Wanafunzi na wala haikusema kuwa ujauzito ni sababu halali za kuondolewa shule kabisa, Sheria hiyo ilimpa waziri mamlaka ya kuunda sera ambazo 'Ataona yafaa kutekeleza'

Hatimaye mwaka 2002 serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Elimu na kuingiza kifungu kilichokuwa kinaruhusu kuondolewa shule kwa Mwanafunzi yoyote ambaye atakuwa amefanya makosa ya dhidi ya ukiukwaji wa maadili. Kifungu hiki cha sheria ndicho kilichopelekea waofisa mbalimbali katika ngazi ya elimu watoe tafsiri ya kuwa Kupata Ujauzito nalo ni kosa dhidi ya maadili, licha ya wao kutambua mabinti zaidi ya asilimia 36 walikuwa wakiolewa wakiwa chini ya miaka 14 kikiwa kiwango kikubwa kabisa katika nchi zote duniani, hivyo kufanya sheria hii kuwa kandamizi.

Mnamo mwaka 2009 Tanzania ilitunga Sheria ya Haki ya Mtoto, ikibainisha haki ya mtoto kuhudhuria shule, bila kujali jinsia au mazingira. Licha ya hayo, kufukuzwa kuliendelea kwa kasi ya rekodi. Inakadiria kuwa zaidi ya wasichana 8,000 huacha shule au kufukuzwa kwa ujauzito kila mwaka. https://www.bbc.com/swahili/habari-48677683 Mashirika mbalimbali ya haki za binadamu yanachukulia sera hii ya Tanzania kama ukiukaji wa moja kwa moja wa sheria zake za elimu na mikataba ya kimataifa waliyokubali kuidhinisha.

Hatimaye mwaka 2017, Hayati Magufuli aliahidi kwamba hakuna mwanafunzi atakayepata ujauzito ambaye atamaliza masomo yake chini ya utawala wake, akisema ni kinyume cha maadili kwa wasichana wadogo kufanya ngono.

*"Ninatoa pesa kwa Mwanafunzi kusoma bure. Na kisha, anapata mimba, anajifungua na baada ya hapo, anarudi shuleni. Hapana, sio chini ya mamlaka yangu,"*

RAIS MAGUFULI APIGA MARUFUKU WANAOPATA MIMBA KUENDELEA NA SH…

Kauli hii ndio iliyoleta shida kubwa kwa watoto wa kike nchini kwa kupimwa mimba katika mazingira ya kidhalilishaji, kufukuzwa shule na wengi wamekosa nafsi ya kuelimika, kutokana na kauli ya Rais Magufuli kwamba hatosomesha malaya kwa fedha za serikali, lakini pia akazieleza NGOs na watetezi wa watoto kupata elimu kama wanataka basi wajenge shule zao wakawasomeshe huko.

Watoto wa kike walikosa utetezi wa kutosha, wakafukuzwa shule, lakini walijitokeza wachache kama wanaharakati na NGO kuwatetea watoto wa kike ili wapate nafasi ya kuelimika, kutokana na kauli ya Rais Magufuli kwamba hatosomesha malaya kwa fedha za serikali, lakini pia akazieleza NGOs na watetezi wa watoto kupata elimu kama wanataka basi wajenga mashule yao wakawasomeshe huko.

Watoto wa kike walikosa utetezi wa kutosha, wakafukuzwa shule, lakini walijitokeza wachache kama wanaharakati na NGOs ambazo ziliomba umma na makundi mbalimbali ya haki za wanawake kufungua kesi mahakamani dhidi ya Tanzania kwa kuendeleza vitendo viovu.

Mnamo mwaka wa 2019, Waziri wa Elimu wa Tanzania alitangaza kwamba wasichana wa shule waliopata mimba wanaweza kuendelea na masomo, lakini si kupitia mfumo wa elimu rasmi . Benki ya Dunia iliipatia Tanzania mkopo wa dola milioni 500 kujenga shule hizo mbadala chini ya Mpango wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).http://idc-tz.org/news/secondary-education-quality-improvement-project-sequip

Hata hivyo suala hili lilipingwa vikali na taasisi mbalimbali na wanaharakati wa haki za wanawake nchini, kwani waliona kama ubaguzi kuwatengenezea mfumo wa nje zaidi ya ule uliozoeleka. (Mfumo wa elimu)
https://www.hrw.org/news/2021/10/06/tanzania-pregnant-student-ban-harms-thousands

Novemba 24, 2021, Wizara ya Elimu ya Tanzania ilipitisha Waraka Na. 2 wa 2021 https://bit.ly/3d1tcCV kuhusu kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo ya sekondari, unaoeleza mahususi haki ya akina mama vijana kurejea katika shule za umma na kutoa maelekezo kwa shule kuchukua wanafunzi hao. Uamuzi huu unahitimisha kikamilifu marufuku ya shule kwa Tanzania dhidi ya wanafunzi waliopata ujauzito, na kuiweka Tanzania katika kundi la nchi ambazo Human Rights Watch imepata kuwa
"Zimeondoa sera zenye vikwazo hivi karibuni, lakini zina pengo la kisera" https://www.hrw.org/news/2022/04/01/tanzania-allows-teenage-mothers-be-back-school

Pengo hili la kisera linatokana na ukweli kwamba licha ya serikali kuruhusu wanafunzi waliopata ujauzito kurudi shule hakuna utaratibu maalum uliowekwa kisheria na kisera kwa namna gani wanafunzi hawa watarudi shule. Hata hivyo imeonakana kama ni matakmko ambayo yametolewa tu na serikali ili kuridhisha umma, wafadhili kama benki ya dunia na nchi washirika. Hali ipo tofauti kwa upande wa Zanzibar, ambapo Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi mmoja Namba 4 ya mwaka 2005 http://idc-tz.org/news/the-spinsters-and-single-parent-children-protection-act-2005 imeruhusu Wanafunzi waliopata ujauzito kuendelea na Elimu yao katika mfumo wa kawaida. Sheria hii imeleta mabadiliko makubwa na ukombozi mkubwa kwa watoto waliopata ujauzito.

Mapendekezo

Serikali inapaswa kurekebisha Sheria ya Elimu, na kurekebisha Kanuni za Elimu za 2002 (Expulsion and Exclusion of Pupils from Schools) na nyingine zinazo ambatana nazo, na kuweka ulinzi kwa wanafunzi wajawazito. https://necta.go.tz/files/SERA2.pdf

Pia Serikali inapaswa kupitisha kwa Haraka sera ya kitaifa ya kuendelea, miongozo ya shule, na mtaala wa kitaifa wa elimu ya uzazi.